

bidhaa au huduma kwa njia ya kielektroniki au mtandao. Vigezo hivi vinamsaidia mlaji ili aweze kupata bidhaa kwa viwango anavyohitaji.

Sheria pia imempa mlaji nguvu ya kisheria kukagua bidhaa, kurekebisha makosa yoyote kwenye bidhaa husika au kukataa muamala wowote wa mauzo iwapo hajakubalina na viwango vya bidhaa husika.

2.10 Uwepo wa Mnada kwa Njia ya Mtandao

Sheria imeanisha namna ya ununuzi wa bidhaa au huduma kwa mnada kwa njia ya kielektroniki. Kwa mujibu wa sheria hii, mshindi wa mnada unaofanyika kwa njia ya kielektroniki atapatikana pale atakapokuwa ameweka dau kubwa kuzidi wengine kabla ya kuisha kwa muda uliokubaliwa.

3.0 HITIMISHO

Sheria ya Miamala ya Kielektroniki imeweka msingi wa mabadiliko ya utendaji katika masuala mbalimbali na hivyo kurahisisha utekelezaji wake. Mabadiliko haya ni muhimu katika kushamirisha shughuli za kiuchumi na utoaji wa huduma mbalimbali.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



Kwa maoni wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo:

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria
Tanzania,

Jengo la Taaluma Na. 1,
Barabara ya Mkalama
S.L.P. 1718
DODOMA,
TANZANIA

Barua pepe: lrc@lrc.or.tz
Tovuti: www.lrc.go.tz

SHERIA YA MIAMALA YA KIELEKTRONIKI



1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171. Kwa mujibu wa sheria hii pamoja na mambo mengine Tume inajukumu la kufanya mapitio ya sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuzwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia.

Katika kutekeleza jukumu hili, Tume imefanya mapitio na kuandaa Taarifa ya Mfumo wa Sheria Unaohusu Biashara Mtandaoni na Makosa ya Mtandaoni ya Mwaka, 2006.

2.0 SHERIA YA MIAMALA YA KIELEKTRONIKI NA. 6 YA 2015

Sheria ya Miamala ya Kielektroniki pamoja na masuala mengine imeainisha yafuatayo:

2.1 Utambuzi wa Miamala ya Kielektroniki

Sheria imeelekeza kutoa ujumbe au taarifa yoyote ya kielektroniki itakuwa ni halali na yenye nguvu ya kisheria.

2.2 Uhalali wa Miamala ya Kielektroniki

Sheria inatoa vigezo ambavyo miamala yoyote ambayo haikuwa kwenye mfumo wa kielektroniki inaweza kukubalika kwa njia ya kielektroniki. Hivyo kuleta uhalali wa miamala inayofanyika kwa njia ya kielektroniki.

2.3 Saini za Kielektroniki

Sheria inaainisha vigezo vya kuzingatwa kwenye matumizi ya saini za kielektroniki. Vigezo hivyo ni pamoja na uhalali wa saini kumtambulisha mhusika na uhalali wa matumizi ya saini kwenye muamala husika. Pia inaainisha zaidi kuwa, kwenye mikataba, wahusika wanaweza kukubalika namna fulani ili iweze kutumika kama saini katika miamala kwa mujibu wa mkataba husika.

2.4 Uthibitisho wa Mtu au Nyaraka Mbalimbali za Kisheria

Sheria imeelekeza kuwa iwapo mtu yeyote atahitaji kutoa uthibitisho wake wa kisheria kwa njia ya kielektroniki, itamlazimu mtu huyo kuweka saini yake ya kielektroniki.

Iwapo ni uthibitishwaji wa nakala za nyaraka mbalimbali za kisheria ambazo ni za kielektroniki, itamlazimu mtu huyo kuchapisha nakala za nyaraka husika ya kielektroniki na kisha kuthibitishwa kisheria.

2.5 Utambuzi wa Huduma za Serikali mtandao

Sheria inaweka bayana kuwa taasisi yoyote ya serikali inaweza kutoa nyaraka au huduma yoyote kwa wananchi kwa njia ya kielektroniki.

2.6 Malipo kwa Njia ya Mtandao

Kupitia sheria hii pamoja na sheria zingine za malipo ya fedha, huduma ya malipo kwa njia ya kielektroniki au mtandao inapatikana kwenye huduma mbalimbali binafsi na za kiserikali.

2.7 Kukubalika kwa Ushahidi wa Kielektroniki Mahakamani

Sheria inaruhusu ushahidi wa kielektroniki kukubalika na kupokelewa mahakamani. Vigezo hivyo ni pamoja na uhalali wa jinsi ushahidi wa kielektroniki ulivyoandaliwa, ulivyotunzwa na ulivyowasilishwa. Ushahidi huu, unahusisha vielelezo vitakavyowasilishwa mahakamani kwa njia ya kielektroniki.

Sheria imeanisha vigezo na mazingira ya kukubali ushahidi wa kielektroniki na uwasilishwaji wake mahakamani. Ushahidi wa aina hii utakubalika na kuwasilishwa mahakamani iwapo haujagushiwa.

2.8 Utambuzi wa mikataba ya Kielektroniki

Sheria inaruhusu wahusika kwenye mkataba kuingia mkataba kwa njia ya kielektroniki. Sheria hii imeanisha mazingira na vigezo vya namna ya kufunga mikataba baina ya wahusika kwa njia ya kielektroniki au mtandao. Miongoni mwa mazingira na vigezo vya kuingia mkataba wa kielektroniki ni uhalali wa mkataba wenyewe, kupokelewa kwa mkataba wa kielektroniki, sehemu ambayo mkataba ulitumwa na kupokelewa kielektroniki na muda na mahali ambayo wahusika waliingia mkataba wa kielektroniki.

2.9 Biashara kwa Njia ya Kielektroniki na Ulinzi wa Mlaji

Kwa kutambua uwepo wa biashara mtandao, sheria imeanisha vigezo vya msambazaji kuzingatia iwapo atafanya biashara ya